# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA SABA

**16 APRILI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA SABA – TAREHE 16 APRILI, 2025

## I. DUA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA FEDHA:**

(i) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Central Government for the Financial Year 2023/24);*

(ii) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Local Government Authorities for the Financial Year 2023/24);*

(iii) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Development Projects for the Financial Year 2023/24);*

(iv) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of the Public Authorities and Other Bodies for the Financial Year 2023/24);*

(v) Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalum kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Disemba, 2024 *(The Annual General Report on the Performance and Specialised Audits for the Period Ending 31st December, 2024) ;*

(vi) Ripoti Kuu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2024 *(The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Information Systems for the Financial Year 2023/24);*

(vii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Huduma za Vivuko (*Performance Audit Report on the Management of Ferry Operations);*

(viii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Baharini (*Performance Audit on the Regulation of Maritime Transport Services);*

(ix) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Msaada na Udhibiti wa Tiba za Asili *(Performance Audit Report on the Provision of Support and Regulation of Traditional Medicine);*

(x) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Utoaji wa Vyeti vya Vizazi na Vifo *(Performance Audit Report on the Identification, Registration and Issuance of Birth and Death Certificates);*

(xi) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Data za Kijiosayansi katika Sekta ya Uchimbaji Madini *(Performance Audit Report on the Management of Geoscientific Data in the Mining Sector);*

(xii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Mradi wa Kujenga Kesho Bora – Mpango wa Vijana kwa Biashara ya Kilimo (BBT-YIA) *(Performance Audit Report on the Implementation of Building a Better Tomorrow – Youth Initiative for Agribusiness (BBT-YIA));*

(xiii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utoaji wa Huduma za Ugani kwa Rasilimali za Mifugo *(Performance Audit Report on the Provision of Extension Services to Livestock Resources);*

(xiv) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Huduma za Hali ya Hewa *(Performance Audit Report on the Management of Meteorological Services);*

(xv) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Vifaa vya Kielekitroni vya Kodi katika Kukusanya Mapato *(Performance Audit Report on the Management of Electronic Fiscal Devices (EFDs) in Revenue Collection);*

(xvi) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Biashara ya Kaboni *(Performance Audit Report on the Management of Carbon Trade);*

(xvii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Kukabiliana na Hali ya Jangwa *(Performance Audit Report on the Implementation of the National Action Plan for Combating Desertification);*

(xviii) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi na Matumizi ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano katika Mamlaka za Udhibiti katika Utoaji wa Huduma za Udhibiti *(Performance Audit Report on the Management*

*and Utilization of ICT in Regulatory Authorities in the Delivery of Regulatory Services);*

(xix) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Gharama za Mifumo ya TEHAMA ya Serikali iliyotengenezwa Ndani *(Performance Audit Report on Cost-effectiveness of Internally Developed Government ICT System);*

(xx) Taarifa ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu Usimamizi wa Mafuriko *(Performance Audit Report on the Management of Floods);* na

(xxi) Taarifa ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kaguzi za Ufanisi zilizofanyika na Kuwasilishwa Bungeni Mwaka 2021 *(Follow-up Report on the Implementation of the Controller and Auditor General's Recommendations from the Fourteen Performance Audit Reports Issued and Tabled to the Parliament in April, 2021).*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

## III. MASWALI:

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**82. MHESHIMIWA MUNIRA MUSTAPHA KHATIB (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongeza idadi ya Madaktari na Wauguzi hasa maeneo ya Vijijini.

**83. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA CHOMETE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini katika Kituo cha Afya Ilamba Wanawake na Watoto wanalazwa katika Wodi moja.

**84. MHESHIMIWA PAULINE PHILIPO GEKUL (BABATI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ipi kauli ya Serikali kwa Wakulima na Wafanyabiashara kulipishwa *crop cecy* zaidi ya mara moja wanapovusha mazao Halmashauri nyingine.

**85. MHESHIMIWA REHEMA JUMA MIGILLA (ULYANKULU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itafanya ukarabati wa Shule za Msingi Taba, Mkindo, Kaswa, Mbeta na Milambo.

**86. MHESHIMIWA STEPHEN LUJWAHUKA BYABATO (BUKOBA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Barabara ya Lake Oil - Ijuganyodo hadi Kyamunene itajengwa kwa kiwango cha lami.

**OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):**

**87. MHESHIMIWA DKT. ALICE KARUNGI KAIJAGE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kufuatilia Waajiri ili wawe wanatoa mafunzo kwa Watumishi kabla ya kustaafu.

**WIZARA YA NISHATI:**

**88. MHESHIMIWA IDDI KASSIM IDDI (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaunganishia umeme Wateja waliolipia kabla ya mabadiliko ya bei katika Halmashauri ya Msalala.

**WIZARA YA KILIMO:**

**89. MHESHIMIWA JOSEPH GEORGE KAKUNDA (SIKONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itawawezesha Wakulima wasio na fedha taslimu kupata mikopo ya mbolea ya ruzuku.

**90. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (BLW):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali imewezaje kutatua changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP 1).

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**91. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, kuna mpango gani wa kupeleka Meli ya Uvuvi Ziwa Nyasa ili kuvua Samaki wanaoishi kwenye kina kirefu ambao kwa sasa wanakufa kwa uzee.

**WIZARA YA FEDHA:**

**92. MHESHIMIWA KATANI AHMAD KATANI (TANDAHIMBA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, lini Serikali itarejesha fedha za Miradi iliyochukuliwa na Hazina ili miradi hiyo iweze kukamilishwa.

## WIZARA YA AFYA:

**93. MHESHIMIWA AYSHAROSE NDOGHOLI MATTEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida.

**94. MHESHIMIWA NANCY HASSAN NYALUSI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza tatizo la udumavu nchini.

**95. MHESHIMIWA LUCY JOHN SABU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, kuna mpango gani wa kuongeza Vituo vya Ushauri na Programu za uhamasishaji ili kusaidia Vijana na tatizo la Afya ya Akili.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

### WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**DODOMA**
**16 APRILI, 2025**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**